Suluhisho la Shida

Sura ya 9
Somo la Kusikiza: Agano la Kale #54

Shabaha: Kujifunza kuhusu Zaburi za kihisia na vile zinaweza tuzaidia kuweza maangaiko ya kila siku.

Ee Mungu wa haki yangu, uniitikie niitapo; umenifanyizia nafasi wakati wa shida; unifadhili na kuisikia sala yangu. Wengi husema nani atakayetuonyesha mema? BWANA utuinulie nuru ya uso wako. Umenitia furaha moyoni mwangu, kupita yao wanapozidishiwa nafaka na divai. Katika amani nitajilaza na kupata usingizi mara, maana wewe BWANA peke yako ndiwe unijaliaye kukaa salama.

- Zaburi 4:1, 6-8

Umtwike BWANA mzigo wako naye atakutegemeza. Hatamwacha mwenye haki aondoshwe milele. Nawe Ee Mungu, utawatelemsha walifikilie shimo la uharibifu; watu wa damu na hila hawataishi nusu ya siku zao, bali mimi nitakutumaini wewe.

- Zaburi 55:22-23

Zaburi zilizo na mada ya hisia huwa mara nyingi ni zaburi za maombi, mahali ambapo mtunga zaburi anaongea na Mungu kuhusu wanadamu – mara nyingi yeye mwenyewe. Zaburi hizi zinatufunza kuwa tukileta hisia zetu za mashaka, uwoga, hasira, kufunjika moyo, kukosa tumaini au kitu kingine chochote kwa Mungu, yeye hutusaidia kupitia hisia hizo na kutuongoza ndani ya shukrani na kuabudu. Zaburi hizi zinatufunza kuwa Mungu huturuhuzu kumwongelesha kuhusu chochote, hata hisia zetu za kinyume, kwa sababu yeye ana haja na sisi. Hutusikia na kutujibu tunapokuwa na mazungumzo naye. Tunapopata majibu kutoka kwake, tunapaswa kutiwa moyo sana. Maisha hayapaswi kuwa kawaida tena.

Wakati tunapitia hali ya kufinyika kihisia, tunaweza pata kila mara zaburi inayoongea juu ya hisia kama hiyo ya kufinyika. Mazungumzo na Mungu yaliyoandikwa na Daudi na wanazaburi wengine ni miongozo ya muhimu zaidi kwa mazungumzo yetu na Mungu. Tunaweza fuata mifano yao na kupata pumziko, tumaini na amani ya kushinda shida zetu.

1. Ukweli au uongo? Zaburi za maombi kila mara zimejaa hisia.

2. Ukweli au uongo? Kufadhaika hakupatikani katika zaburi kwa sababu ni ishara ya utoto wa kiroho?

3. Ukweli au uongo? Mungu anataka maombi yetu yawe mazungumzo ya pande zote mbili sisi na yeye.

Ikiwa hujaambiwa lingine la kufanya, basi, chagua jibu moja tu kwa kila swali lifuatalo.

4. Mungu huitikia vipi tunapomwambia kuhusu taabu zetu?
    a. Anakataa kutusikiza
    b. Anatusikia na kutuhudumia
    c. Anatwambia inafaa tuwe watu wa nguvu zaidi
    d. Anatwambia tufikirie zaidi juu ya uwezekano

5. Inadhibitisha nini Mungu anapojibu maombi yetu.
    a. Kuwa anatujali na hushughulikia mahitaji yetu
    b. Kuwa atatupa tunachokihitaji ili kuzima malalamiko yetu kwake
    c. Kuwa tumemfurahisha na ukomavu wetu
    d. Kuwa tulisema maneno sahihi

6. Ni nini sehemu muhimu ya mazungumzo yetu na Mungu?
    a. Tunapomwambia mahitaji yetu
    b. Tunapowaombea watu wengine
    c. Tunapokiri dhambi zetu
    d. Anapoongea nasi

7. Tunapoamua kufanya yaliyo sawa na kumtumainia Mungu, matokeo yake ni nini?
    a. Kufunjika moyo na kuudhika
    b. Utajiri na fahari
    c. Furaha na amani
    d. Maumivu na ufukara

(Kiongozi soma Zaburi 55)

8. Ni hisia gani ambazo Daudi alionyesha alipoandika Zaburi 55? *(Chagua yote yaliyo sahihi)*
    a. Huzuni
    b. Amani
    c. Utiifu
    d. Hasira
    e. Uwoga
    f. Uvumilivu
    g. Uchungu

9. Ni hisia na nia ya aina gani ambayo Mungu anakubali tumletee? *(chagua yote yaliyo sahihi)*
    a. Huzuni
    b. Amani
    c. Utiifu
    d. Hasira
    e. Uwoga
    f. Uvumilivu
    g. Uchungu
    h. Yoyote

10. Biblia inatwambia tufanye nini na mizigo yetu?
    a. Tuzibebe wenyewe tu
    b. Tuziache nyuma
    c. Tuwabebeshe wengine
    d. Tumtwike BWANA

11. Tunaweza kuja kwa BWANA lini?
    a. Tukiwa na mizigo mizito tu
    b. Hatuwezi. Ni watu watakatifu na wenye haki tu wanaoweza
    c. Wakati wowote na shida yoyote iwe kubwa au ndogo
    d. Wakati fulani tunapohitaji msaada.

12. Tunapaswa kufanya nini tukiwa na shida na matatizo? *(Chagua yote yaliyosahihi)*
    a. Lalamika
    b. Omba
    c. Jaribu kusahau
    d. Kuwa na hasira
    e. Sikiza Mungu
    f. Kuwa mwenye nguvu na usiruhuzu mtu yeyote kujua
    g. Fanya kilicho sawa

Umewahi kumwomba Mungu wakati unasumbuka? Ilikuwa vipi rahisi au ngumu kumwambia namna ulivyokuwa unahisi? Ni katika njia gani alizojibu?

_____

_____

_____

Kwa hisia zote na nia zote unazopitia maishani leo, mwambia Mungu kuzihuzu na umuulize akusaidie kumtumainia. Mshukuru kwa kukusikia na kuahidi kujibu.

KUZAMA ZAIDI

1. Ni hisia gani alizokuwa nazo mwandishi wa Zaburi nne? _____
_____
_____
_____

2. Alimaanisha nini aliposema kuwa aliongea na moyo wake mwenyewe? _____
_____
_____
_____

3. Ni nini alichoamua kufanya kikabadilisha hisia zake na kumpa amani na usingizi?
_____
_____
_____

4. Maana ya kutoa dhabihu za haki na kuweka tumaini lako kwa BWANA ni nini? _____
_____
_____
_____

5. Ni nini kilichomchochea kufanya uamuzi huo? _____
_____
_____
_____

6. Ni hisia gani alizokuwa nazo Daudi alipoandika Zaburi 55, alifanya nini na hisia hizo, na alitwambia kufanya nini tukiwa na hisia kama hizo? _____
_____
_____
_____

7. Unapokutana na wewe mwenyewe kihisia na kwa kuona zaburi hizi, ni katika njia gani zinakuonyesha maelezo ya hizo hisia? _____
_____
_____
_____